

Spika wa Bunge afurahishwa, mafunzo ya huduma za biashara yanayotolewa na PASS

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson, ameipongeza Taasisi ya PASS Trust kwa namna inavyotoa mafunzo ya uendeshaji wa biashara za mazao ya kilimo ikiwemo ufungaji wa mazao katika vifungashio mbalimbali.

Akizungumza alipotembelea banda la PASS kwenye maonesho ya 29 ya Nane nane, Kitaifa katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya, Tulia alieleza kuridhishwa kwake na jinsi vijana wajasiriamali wa kilimobiashara wanaopata mafunzo katika kituo atamizi cha Ubunifu wa Kilimobiashara kwa Vijana cha PASS-AIC, wanavyofungasha mazao yao.

"Nimefurahishwa sana na jinsi PASS mnavyotoa mafunzo ya kufungasha bidhaa za mazao ya kilimo, huu ndio utaratibu mzuri unaopaswa kufuatwa na taasisi na wazalishaji wote" alisema Dkt. Tulia huku akiitaka PASS Trust kueneza elimu hiyo kwa wadau mbalimbali inafanya nao kazi ili kufikia lengo la serikali kwa wadsau wa kilimo kuacha ufungaji wa rumbesa kama ilivyogaohizwa na Makamu wa Rais wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango alipokuwa akizindua maonesho hayo.

Aidha, ameridhishwa na jinsi PASS inavyoa huduma mbalimbali katika kutatua changamoto za wajasiriamali wa kilimo, mifugo na uvuvi ikiwemo, dhamana za mikopo kutoka katika taasisi za fedha, maandiko ya miradi ya biashara, uatamizi wa vijana Pamoja na mikopo ya zana za kilimo na viwanda inayotolewa na Kampuni tanzu ya PASS Leasing.

Spika huyo wa Bunge ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini, alitumia fursa hiyo kuitaka PASS kuwezesha zao la Karoti ambalo alibainisha kuwa linazalishwa kwa wingi katika mkoa huo.

"Kwakuwa ninyi mnajihuisha na huduma mbalimbali katika sekta ya kilimo, niwaombe pia wekezeni Zaidi katika uwezeshaji wa zao la karoti ambalo linalimwa kwa wingi katika Mkoa wetu wa Mbeya ili kuwapa fursa wananchi kunufaika na zao hili" aliongeza Dkt. Tulia.



Spika wa Bunge la Tanzania, Dkt. Tulia Ackson akiangalia huduma na bidhaa ndani ya banda la PASS katika maonesho ya Nane nane, jijini Mbeya.



Taasisi ya PASS Trust, kupitia huduma zake, imekuwa kiungpo muhimu sana katika kuchagiza maendeleo ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kwani tangun kuanzishwa kwake mwaka 2002 hadi mwezi septemba mwaka 2021, imewezesha mikopo jumuishi takriban Trilioni 1.2 ambayo imedhamini 31% ya mikopo yote ya kilimo nchini na kuwezesha kutengeneza ajira mpya milioni 2.6 na kuwanufaisha wanawake

milioni 1.3 nchini kote.

Akizungumza katika maonesho hayo, Mkurugenzi wa Biashara wa PASS Trust, Adam Kamanda alimueleza Spika wa Bunge kuwa PASS Trust imejidhatiti katika kukabili changamoto zinazowakumba wakulima katika kupata huduma muhimu ikiwemo mikopo ya fedha, maandiko ya miradi Pamoja na ujuzio wa kilimo cha kisasa kinachoendana na mabadiliko ya tabia nchi.